

**MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA
TAREHE 18/11/2016 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI
YA WILAYA YA BUNDA.**

WAJUMBE WALIOHUDHURIA

NA.	JINA	WADHIFA
1.	Mhe. Sabatho M. Mafwimbo	Diwani Kata ya Nansimo - Mwenyekiti
2.	Mhe. Abiud M. Chacha	Diwani Kata ya Butimba - Mjumbe
3.	Mhe. Fedson Rwesunga	Diwani Kata ya Nampindi - Mjumbe
4.	Mhe. Mganga G. Jongora	Diwani Kata ya Mugeta - Mjumbe
5.	Mhe. Merchant K. Ikungura	Diwani Kata ya Salama - Mjumbe
6.	Mhe. Jofrey H. Rashidi	Diwani Kata ya Chitengule - Mjumbe
7.	Mhe. Sophia B. Makamulo	Diwani V/Maalum - Mjumbe
8.	Mhe. Nyachiro C. Chitema	Diwani V/Maalum - Mjumbe
9.	Mhe. Keremba J. Irobi	Diwani Kata ya Nyamang'uta - Mjumbe
10.	Mhe. Mramba S. Nyamkinda	Diwani Kata ya Ketare - Mjumbe
11.	Mhe. Paul N. Kafumu	Diwani Kata ya Igundu - Mjumbe
12.	Mhe. Ruth. W. Mtani	Diwani V/Maalum - Mjumbe
13.	Mhe. Alex P. Msege	Diwani Kata ya Kasuguti - Mjumbe
14.	Mhe. Jogoro A. Biswalo	Diwani Kata ya Namhula - Mjumbe
15.	Mhe. Renatus B. Karoli	Diwani Kata ya Kibara - Mjumbe
16.	Mhe. Majura. E. Majura	Diwani Kata ya Iramba - Mjumbe
17.	Mhe. Misana S. Jigwila	Diwani Kata ya Kisorya - Mjumbe
18.	Mhe. Nyamtondo O. Deus	Diwani V/Maalum - Mjumbe
19.	Mhe. Mgendi P. Kwaye	Diwani Kata ya Nyamiholo - Mjumbe
20.	Mhe. Nyambura Nyasonge	Diwani Kata ya Mihingo - Mjumbe
21.	Mhe. Maria Nyamoko	Diwani V/Maalum - Mjumbe
22.	Mhe. Mariam Sindano	Diwani V/Maalum - Mjumbe
23.	Mhe. Makima H. Josephat	Diwani Kata ya Hunyari - Mjumbe
24.	Mhe. Godliver S. Masamaki	Diwani V/ Maalum - Mjumbe
25.	Mhe. Fyeka S. Sumera	Diwani Kata ya Nyamuswa - Mjumbe
26.	Mhe. Kangi Lugora	Mbunge Jimbo la Mwibara - Mjumbe
27.	Mhe. Boniphace Getere	Mbunge Jimbo la Bunda - Mjumbe
28.	Mhe. Berynice J. Bitta	Diwani V/Maalum - Mjumbe

WAJUMBE WASIOHUDHURIA.

NA.	JINA	WADHIFA
1.	Mhe. Isack M. Kabugu	Diwani Kata ya Neruma - Mwenyekiti wa Halmashauri - kwa taarifa

WAKUU WA IDARA/VITENGO WALIOHUDHURIA

NA.	JINA KAMILI	WADHIFA
1.	Ndg. Dinah L.T.K Rweyemamu	Kny: Mkurugenzi Mtendaji (W) - Katibu
2.	Ndg. Tumaini Magesa	Afisa Utawala Bora (W)
3.	Ndg. Kelvin Mkirya	Kaimu Afisa Rasilimali Watu (W)
4.	Dkt. C.B. Rugakingira	Kaimu Mganga Mkuu (W)
5.	Ndg. Masamba C.F	Mkaguzi wa Ndani (W)

6.	Ndg. Makuke A.L	Kaimu Afisa Tarafa Kenkombyo
7.	Ndg. Blasius O. Ogola	Kaimu Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W)
8.	Ndg. Daud P. Mongo	Kaimu Afisa Mazingira na Udhhibiti wa Taka Ngumu (W)
9.	Ndg. Charles Mushi	Afisa Usafirishaji (W)
10.	Ndg. Julieth Ntuku	Afisa Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji (W)
11.	Ndg. Andrew B. Maregesi	Kaimu Afisa Nyuki (W)
12.	Ndg. Laurent M. Marashi	Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W)
13.	Ndg. Jonas E. Nyeoja	Afisa Tarafa Nansimo
14.	Ndg. Samson Manjale	Kaimu Afisa Manunuzi (W)
15.	Ndg. Sistaimelda Lubengo	Afisa Elimu Msingi (W)
16.	Ndg. Tanu Deule	Mhandisi wa Maji na Udhhibiti wa Maji Taka (W)
17.	Ndg. Benedict Lyamuya	Mweka Hazina (W)
18.	Ndg. Martin Nkwabi	Afisa Elimu Sekondari (W)
19.	Ndg. Arphaxad Miyaye	Kny. Katibu Tawala (W)

WAANDISHI WA HABARI WALIOKUWEPO.

NA	JINA KAMILI	CHOMBO CHA HABARI
1.	Ndg. Raphael J. Okello	Gazeti la Majira/Mtanzania
2.	Ndg. Ahmed Makongo	RFA/Star TV
3.	Ndg. Christopher Maregesi	Gazeti la Mwananchi, Redio One Sterio na ITV
4.	Ndg. Teddy Thomas	Radio Mazingira FM
5.	Ndg. Joseph Manyonyi	Mtanzania

WAGENI WAALIKWA WALIOKUWEPO.

NA	JINA KAMILI	WADHIFA
1.	Mhandisi Juma H. Sementa	Kamishna Msaidizi wa Madini Kanda ya ziwa Victoria

SEKRETARIETI.

NA.	JINA KAMILI	WADHIFA
1.	Ndg. Pereus R. Kyaruzi	Katibu wa Kamati (W)
2.	Ndg. Pili A. Masaza	Katibu wa Kamati Msaidizi
3.	Ndg. Amos J. Kaunya	Katibu wa Kamati Msaidizi.

Ajenda za mkutano wa tarehe 18/11/2016.

- 1 Kufungua mkutano.
- 2 Kuridhia ajenda.
- 3 Maswali ya papo kwa papo.
- 4 Hoja/Maswali.
- 5 Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa mkutano wa Baraza la tarehe 19/08/2016.
- 6 Yatokanayo na mkutano wa Baraza la tarehe 19/08/2016.
- 7 Taarifa za Kamati za Kudumu za Halmashauri.
 - (i) Taarifa ya Kamati ya Kudhibiti UKIMWI.
 - (ii) Taarifa ya Kamati ya Elimu, Afya na Maji.
 - (iii) Taarifa ya Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira.
 - (iv) Taarifa ya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango.

- 8 Taarifa mbalimbali.
 - Matumizi ya magari ya Halmashauri.
- 9 Kufunga mkutano.

MUHTASARI NA. HW/BRZ/2016-2017/01/1 KUFUNGUA MKUTANO.

- 4.1 Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue mkutano.
- 4.2 Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe wote, wageni waalikwa, waandishi wa habari pamoja na wataalam waliohudhuria katika mkutano huo.
 - 4.2.1 Alisema kuwa huu ni mkutano wa Madiwani wa kawaida wa robo ya I mwaka ya 2016/2017.
 - 4.2.2 Aliwaomba wajumbe wa mkutano huo kuwa wasikivu ili kuweza kujadili hoja mbalimbali kwa umakini mkubwa.
 - 4.2.3 Alifungua mkutano saa 4:11 asubuhi.

MUHTASARI NA. HW/BRZ/2016-2017/01/2 KURIDHIA AJENDA.

- 5.1 Ajenda tisa (09) ziliwasilishwa kwenye mkutano.
- 5.2 Wajumbe walizipokea ajenda zote tisa (09) kuwa zijadiliwe katika mkutano huo.

MUHTASARI NA. HW/BRZ/2016-2017/01/3 MASWALI YA PAPO KWA PAPO.

- 6.1 Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe waliojiorodhesha kuuliza maswali ya Papo kwa papo ili waulize maswali.

6.2 Maswali yalijibiwa kama ifuatavyo:-

- 6.2.1 Mhe. Abiud M. Chacha Diwani wa Kata ya Butimba aliuliza swali lake kama ifuatavyo:-
 - 6.2.1.1 Kwa kuwa manesi wa zahanati ya Bulamba wanagombana kituoni na kushindwa kutoa huduma kwa jamii, je Serikali imechukua hatua gani?
 - 6.2.1.2 Swali hilo lilijibiwa na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) kuwa uongozi wa Halmashauri ulifika katika zahanati ya Bulamba mnamo tarehe 10/11/2016 kwa ajili ya usuluhishi na walikuta kuna kutokuelewana kwa manesi wa zahanati hiyo ambao ni Ndg. Josephine Kazaura na Ndg. Nyamboga Manyani kwa kutuhumiana kuongeaana vibaya mtaani na pia kutoheshimiana kazini na hata wakati mwingine kutoleana maneno ya matusi/yenye lugha za maudhi.
 - 6.2.1.3 Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) iliwaita watuhumiwa hao na wote walipewa nafasi za kujieleza na kutoa kero zao, aidha ofisi iliwasuruhisha na kuwapa onyo la mdomo na kuwakumbusha kufanya kazi kwa kuzingatia maadili ya utumishi wa Umma.
 - 6.2.1.4 Wote kwa pamoja walikiri kutorudia makosa hayo mbele ya viongozi wafuatao:-
 - Dkt. Nelson Malisa – Kaimu Mganga Mkuu (W)
 - Ndg. Fadhili Kanyogoto - DHO
 - Ndg. Elizabeth Boniphace - DRCHCO
 - 6.2.1.4 Aidha, Mhe. Diwani wa Kata ya Butimba alieleza mkutano kuwa kutokana na uzembe wa watumishi hao walishasababisha kifo cha mwananchi mmoja na kuna kipindi walishindwa kufika kazini siku tatu (3) mfululizo, hata hivyo ofisi ya Mkurugenzi haikuwachulia hatua zozote. Alieleza pia kuwa

yawezekana watumishi hao wamefanya kazi katika kituo hicho kwa muda mrefu ndiyo maana wamekuwa na viburi na kutowajibika kazini ipasavyo.

6.2.1.5 Wajumbe walikuwa wakali katika suala hilo ambapo walitaka kujua ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) ilichukua hatua gani baada ya watumishi hao kusababisha kifo cha mwananchi kwa sababu ya uzembe na kutowajibika ipasavyo katika utendaji wa kazi. Walitaka watumishi hao wachukuliwe hatua za Kisheria.

6.2.1.6 Baada ya majadiliano ya kina wajumbe walitoa azimio.

6.2.1.6.1 **AZIMIO.** Mkurugenzi Mtendaji (W) awachukulie hatua za kisheria watumishi wa zahanati ya Butimba Ndg. Josephine Kazaura na Ndg. Nyamboga Manyani kwa kushindwa kutoa huduma kwa mwananchi hadi kusababisha kifo kwa uzembe na kutowajibika ipasavyo kazini.

6.2.2 Mhe. Jofrey H. Rashidi Diwani wa Kata ya Chitengule aliuliza maswali matatu (3) kama ifuatavyo:-

6.2.2.1 (i) Ni hatua gani huchukuliwa kwa Serikali za Vijiji zisizotaka kusoma taarifa ya mapato na matumizi kwa wananchi?

6.2.2.1.1 Swali hilo lilijibiwa na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) kuwa Watendaji wa Vijiji wasiosoma taarifa za mapato na matumizi huandikiwa barua za kujieleza kwa kushindwa kusoma taarifa hizo, Watendaji hao wakiendelea kutosoma taarifa hizo huandikiwa barua za onyo kali na muda mwingine hufunguliwa hati za mashtaka na pia kupendekeza kufukuzwa kazi.

6.2.2.1.2 Hoja hiyo ilifungwa.

6.2.2.2 (ii) Tuliahidiwa kupewa mbegu za mihogo aina ya mkombozi lakini hadi leo hii bado hazijaletwa. Je ni hatua gani zitachukuliwa ili kupata mbegu hizo?

6.2.2.2.1 Swali hilo lilijibiwa na Mkurugenzi Mtendaji (W) kuwa mbegu za mihogo aina ya mkombozi zimeanza kusambazwa leo hii ya tarehe 18/11/2016 katika Kata za Salama, Nyamang'uta na Nyamuswa. Siku ya Jumatatu ya tarehe 21/11/2016 mbegu hizo zitasambazwa katika Kata za Namhula, Iramba, Neruma, Igundu na Chitengule. Vijiji vitakavyohusika vitakuwa vimeteuliwa na wataalam wa Kilimo wa Kata husika. Kila Kata itapata mbegu za kutosha ekari tatu (3) sawa na gunia kumi na mbili (12) za mbegu hizo.

6.2.2.2.2 Hii ilitokana na fedha kidogo zilizopatikana toka katika mfuko wa maafa ambazo ziligawanywa katika Halmashauri mbili yaani Halmashauri ya Wilaya na Mji wa Bunda. Aidha, ucheleweshaji wa usambazaji wa mbegu hizo ulisababishwa na ukosefu wa gari unaoikabili Halmashauri yetu.

6.2.2.2.3 Hoja hiyo ilifungwa.

6.2.3 (iii) Kwa nini Halmashauri isitenge fedha kwa ajili ya kununua mtambo wa kulima barabara badala ya kutumia wakandarasi. Kwa kufanya hivyo Halmashauri inaweza kurekebisha miundombinu yake kwa gharama nafuu.

- 6.2.3.1 Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) alijibu swali hilo kwa kusema kuwa ununuzi wa mitambo hiyo unagharimu kiasi kikubwa cha fedha hivyo Halmashauri haitaweza kununua kwa kutumia fedha za makusanyo ya ndani.
- 6.2.3.1 Mhe. Sabatho Mafwimbo na Mwenyekiti wa Mkutano huo aliuieleza mkutano kuwa fedha zinazoletwa toka wizarani (Road fund) zinakuwa zimeelekezwa katika ujenzi na siyo ununuzi wa mitambo ya kulima barabara.
- 6.2.3.2 Mhe. Keremba Irobi alitoa ushauri katika mkutano huo kuwa wataalam wa Idara ya Mipango kwa kushirikiana na Idara ya Ujenzi wanaweza kuandika andiko kwenye Taasisi mbalimbali kwa lengo la kukopeshwa fedha za ununuzi wa mitambo ya kulima barabara.
- 6.2.2.3.3 Hoja hiyo ilifungwa.

MUHTASARI NA. HW/BRZ/2016-2017/05/4 HOJA NA MASWALI BINAFSI.

7.1 Hakukuwa na hoja na maswali binafsi.

MUHTASARI NA. HW/BRZ/2016-2017/06/5 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO YA TAREHE 19/08/2016.

- 8.1 Muhtasari huo ulisomwa kwenye mkutano.
- 8.2 Wajumbe waliupokea muhtasari huo.
- 8.3 Mwenyekiti na Katibu waliweka saini na kuwa kumbukumbu sahihi za mikutano ya Halmashauri.

MUHTASARI NA. HW/BRZ/2015-2016/05/6 YATOKANAYO NA MKUTANO WA TAREHE 19/08/2016.

- 9.1 Utekelezaji wa maazimio uliwasilishwa kwenye mkutano.
- 9.2 Wajumbe waliupokea utekelezaji huo na kuujadili.

9.3 MAJADILIANO.

- 9.3.1 Kuhusu azimio Na. 1 la Muhtasari Na. HW/BRZ/2015-2016/06/4 Dondoo Na. 43.2.2.2.1 maelezo yalitolewa na Mkaguzi wa Ndani (W) kuwa awali ya yote anaomba radhi kwa kuchelewa kufanya kazi kutokana na maagizo mbalimbali yaliyotolewa na Wahe. Madiwani katika vikao mbalimbali vya Halmashauri sababu kubwa za kutokamilisha maagizo hayo ni zifuatazo:-
- Kudhoofika kiafya kwa kipindi hiki kulikomkata kwa wiki nne mfululizo.
 - Kwa kipindi hiki yuko katika zoezi la uhakiki wa madeni ya watumishi kazi ambayo inahitajika sana Serikali Kuu na rejea agizo la Waziri Mkuu kwa Wakurugenzi wote nchini.
- Aidha alimwomba Mungu awe na afya njema ili baada ya kukamilisha kazi tajwa hapo juu ajitahidi kufanya kazi za maagizo ya Wahe. Madiwani zote kazi ambazo nyingine amekwishazianza ila bado hazijakamilika.
- 9.3.1.1 Wajumbe waliyapokea maelezo hayo na kuagiza kuwa utekelezaji uendeleo na kikao kijacho wapate majibu.
- 9.3.1.2 **AZIMIO.** Mkaguzi wa Ndani (W) afanye ukaguzi wa fedha Tshs. Milioni 10 zilizopelekwa na Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa msingi wa zahanati ya Kabainja Kata ya Kasuguti na atoe mtiririko wa fedha hizo zilivyotumika.

9.3.2 Kuhusu azimio Na. 2 la Muhtasari Na. HW/BRZ/2015-2016/06/7 Dondoo Na. 45.3.3.3.1 lilitekelezwa kwa Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W) kwa kuwasilisha barua isiyokuwa na Kumb. Na. ya tarehe 01/09/2016 yenye kichwa cha barua "Majibu ya hoja Na. HW/BRZ/2015-2016/7".

9.3.2.1 Wajumbe hawakuridhishwa na utekelezaji uliotolewa na Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W) kwani katika utekelezaji huo uliowasilishwa ulikuwa na mapungufu yafuatayo:-

- Barua iliyowasilishwa haikuwa na Kumb. Namba
- Barua haikuonesha bayana kuomba msamaha (Kichwa cha barua hakikujifafanua)
- Mihtasari ya vikao vilivyofanyika haikuwasilishwa.
- Mahudhurio yaliowasilishwa ni yale ya vitabu vya wageni na siyo ya mahudhurio ya vikao vya pembejeo.

9.3.2.2 Wajumbe walijigeuza Kamati ya Madiwani kufuatia kifungu na 34 na 35 cha Kanuni za kudumu za mikutano ya shughuli za Halmashauri zilizotungwa chini ya Kifungu cha 70 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Na. 7 ya mwaka 1982 vimeipa mamlaka Baraza la Madiwani kujigeuza kama Kamati endapo litajitokeza jambo lolote katika kikao cha Halmashauri linalohusu uteuzi, kupandishwa cheo, kufukuzwa kazi, mishahara au mazingira ya kazi au utendaji kazi kwa jumla wa mtumishi yeyote wa Halmashauri, jambo hilo litajadiliwa katika Kamati ya Halmashauri nzima, isipokuwa kama Halmashauri itaamua vinginevyo.

9.3.2.3 Baada ya kujadili kwa kina wajumbe waliona kuna haja ya kuunda Kamati ndogo ili kufuatilia mchakato mzima wa usambazaji wa ruzuku ya pembejeo za kilimo katika Kata ya Namhula.

9.3.2.3.1 **AZIMIO.** Kamati ndogo iliyoungwa kufuatilia mchakato mzima wa usambazaji wa pembejeo za kilimo kwa utaratibu wa vocha kwa mwaka wa fedha 2014/2015 katika Kata ya Namhula iwasilishe utekelezaji huo kwenye mkutano ujao.

Kamati iliundwa kama ifuatavyo:-

NA.	JINA	WADHIFA
1.	Mhe. Makima Josephat	Diwani Kata ya Hunyari
2.	Mhe. Fedson Rwesunga	Diwani Kata ya Nampindi
3.	Mhe. Alex P. Msege	Diwani Kata ya Kasuguti
4.	Mhe. Nyamtondo O. Deus	Diwani Viti Maalum
5.	Mhe. Godliver Masamaki	Diwani Viti Maalum
6.	Ndg. Felista Masamba	Mkaguzi wa Ndani (W)
7.	Ndg. Michael Haule	Mwanasheria (W)

Kamati ilipewa hadidu za rejea kama ifuatavyo:-

- Kuitisha mikutano ya hadhara katika Vijiji vya Kata ya Namhula na wapate fomu za wakulima walivyokuwa wanahudumiwa ikiwa ni pamoja na kuhakiki saini za wanufaika.

- Wapate hati za mapokeo ya pembejeo katika Vijiji vya Namhula.
- Wapate mihtasari ya vikao vya Kamati za vocha.
- Wapate nakala ya vitabu vya vocha.
- Wapate vitabu na stakabadhi za ulipaji wa mchakato mzima wa pembejeo kwa wauzaji wa mawakala.
- Kufanya mahojiano ya ana kwa ana na Ndg. Serapion Rujuguru pamoja na
- Mhe. Jogoro Amon Biswalo pamoja na Watendaji wa Vijiji vya Kata ya Namhula.
- Wapate fomu na orodha ya wanufaika kwenye mikutano ya hadhara.
- Kuwasilisha mapendekezo na ushauri kwenye Mkutano wa Baraza juu ya hoja hiyo.
- Kupitia vielelezo vilivyowasilishwa kwenye Kamati ya Halmashauri na Mhe. Jogoro Amon Biswalo.
- Aidha Mhe. Jogoro Amon Biswalo aiwasilishie Kamati ndogo vielelezo vifuatavyo:-
 - Kielelezo cha mifuko 60 ya mbolea katika Kata ya Namhula.
 - Hati ya vielelezo mifuko 50 ya mpunga.
 - Barua mbili za Mwenyekiti wa Kijiji cha Chingulubila akioneshwa kutoshirikishwa kwenye mchakato huo.

9.3.3 Kuhusu azimio Na. 3 la Muhtasari Na. HW/BRZ/2015-2016/06/7 Dondoo Na. 45.3.3.3.2 lililomtaka Mkaguzi wa Ndani (W) afanye ukaguzi wa usambazaji wa ruzuku za pembejeo za kilimo kwa utaratibu wa vocha katika mwaka wa fedha 2015/2016 ikiwa inaonekana kuna ubadhirifu mkubwa wa fedha zenye thamani ya takribani Tshs. Milioni 60 na watakaothibitika kufanya ubadhirifu huo wachukuliwe hatua stahiki.

9.3.3.1 Maelezo yalitolewa na Mkaguzi wa Ndani kuwa awali ya yote anaomba radhi kwa kuchelewa kufanya kazi kutokana na maagizo mbalimbali yaliyotolewa na Wahe. Madiwani katika vikao mbalimbali vya Halmashauri sababu kubwa za kutokamilisha maagizo hayo ni zifuatazo:-

- Kudhoofika kiafya kwa kipindi hiki kulikomkata kwa wiki nne mfululizo.
- Kwa kipindi hiki yuko katika zoezi la uhakiki wa madeni ya watumishi kazi ambayo inahitajika sana Serikali Kuu na rejea agizo la Waziri Mkuu kwa Wakurugenzi wote nchini.

Aidha alimwomba Mungu awe na afya njema ili baada ya kukamilisha kazi tajwa hapo juu ajitahidi kufanya kazi za maagizo ya Wahe. Madiwani zote kazi ambazo nyingine amekwishazianza ila bado hazijakamilika.

9.3.3.2 Wajumbe waliyapokea maelezo hayo na kuagiza kuwa utekelezaji uendeleo kufanyika kufuatia azimio Na. 2 lenye dondoo Na. 9.3.2.3.1.

9.3.4 Kuhusu azimio Na. 4 la Muhtasari Na. HW/BRZ/2015-2016/06/7 Dondoo Na. 45.3.5.2.1 lilitokelezwa kwa Kaimu Mganga Mkuu (W) kumwandikia barua Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda yenye Kumb. Na. A:20/18/PART III/327 ya tarehe 11/11/2016 iliyohusu tuhuma dhidi ya Hospitali teule ya Wilaya ya Bunda DDH. Iliyoeleza zaidi juu ya hoja binafsi ya Mhe. Fyeka

Sumera Sumera Diwani wa Kata ya Nyamuswa ambaye aliituhumu Hospitali ya Bunda DDH kuwa imekuwa ikitoa huduma za afya chini ya kiwango, imekuwa ikitoa huduma za afya zisizo na uwiano kwa mfano kutoza watoto wenye umri chini ya miaka mitano, mama wajawazito, wazee na wenye magonjwa sugu (wasiojiweza), imekuwa ikiwajali zaidi wateja wa papo kwa papo tofauti na wateja wa huduma nyingine kama NHIF n.k hivyo aliiomba ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda iweze kushughulikia hoja hizo na kuweza kupata ufumbuzi kwa manufaa ya jamii yetu.

9.3.4.1 Wajumbe waliupokea utekelezaji huo, waliujadili kwa kina huku wakigusia juu ya ukosefu wa Kituo cha Afya/Hospitali teule katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda hivyo kupelekea wananchi kukosa huduma stahiki. Waliona kuna haja ya kuteua Kituo cha Afya/Hospitali mojawapo na kuipa hadhi ya kuiendeleza kwa kasi ili itumiwe na Halmashauri ya Wilaya kama Hospitali teule ya Wilaya kati ya Kituo cha Afya Manyamanyama na Hospitali teule ya Bunda DDH ikiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda suala la kuteuwa kituo kimoja kati ya kituo cha afya Ikizu pamoja na Kasahunga havitaweza kuhudumia kwa urahisi wananchi wote wa Wilaya ya Bunda kulingana na jiografia ya Wilaya husika kwani imeundwa na vipande viwili (majimbo) visivyongana

9.3.4.2 Baada ya majadiliano ya kina wajumbe walitoa azimio.

9.3.4.2.1 **AZIMIO.** Mkurugenzi Mtendaji (W) akutane na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda wajadili suala la kuona uwezekano wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda kupata hospitali/kituo cha afya kimojawapo kati ya Hospitali teule ya Bunda DDH na Kituo cha Afya Manyamanyama kitakachosimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Bunda kama Hospitali teule ya Wilaya ikiwa ni pamoja na kumuomba Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda kumtaka Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji wa Bunda kujibu hoja binafsi ya Mhe. Fyeka Sumera Sumera dhidi ya Hospitali teule ya BDDH kwa kuwa hospitali hiyo ipo kwenye Mamlaka ya Halmashauri ya Mji wa Bunda.

Aidha hoja binafsi inahusu maeneo yafuatayo:-

- Huduma hafifu kwa wagonjwa jambo linalopelekea vifo kutokana na uzembe wa watumishi hospitalini hapo.
- Hospitali ya Bunda DDH kuendelea kutoa huduma kama hospitali binafsi pasipo kujali mkataba walioingia na Serikali ili kusaidia mahitaji ya wananchi.
- Hospitali ya Bunda DDH kukaidi agizo la Serikali la kutoa huduma za matibabu bure kwa makundi maalum mathalani wazee wa miaka 60, watoto chini ya miaka 5 na mama wajawazito.
- Hospitali ya Bunda DDH kuonesha ubaguzi wa dhahili kati ya wagonjwa wanaotibiwa kwa kadi za Bima ya Afya na wale wa papo kwa papo.
- Kulipa fedha za dawa kabla ya kutibiwa na kumuona Daktari.

9.3.5 Kuhusu azimio Na. 5 la Muhtasari Na. HW/BRZ/2015-2016/06/7 Dondoo Na. 45.3.5.12.1 lilitekelezwa kwa Mweka Hazina (W) kueleza kuwa zoezi la kukagua na kukusanya ada za leseni za biashara ili kuingizwa kwenye mfumo wa Kielektroniki linaendelea hadi sasa timu ya ukusanyaji wa mapato imekagua biashara 165 katika Kata ya Kibara, biashara 75 katika Kata ya Iramba bado zoezi linaendelea kukagua na kukusanya ada za leseni za biashara katika Kata zilizobaki 17 ili kuingiza kwenye mfumo wa Kielektroniki ifikapo mwezi Desemba, 2016.

9.3.5.1 Wajumbe waliupokea utekelezaji huo na kufunga hoja baada ya kushauri kuwa ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) iwezeshe timu ya ukusanyaji wa mapato ili kuweza kufanya kazi hizo kwa wakati.

9.3.6 Kuhusu azimio Na. 6 la Muhtasari Na. HW/BRZ/2015-2016/06/7 Dondoo Na. 45.3.5.12.1 lilitekelezwa kwa Mwanasheria (W), Afisa Uvuvi (W) pamoja na Mweka Hazina (W) kuwa katika mchakato wa marekebisho ya Sheria ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, mapendekezo ya kubadili viwango vya ushuru wa gunia la dagaa kwa kuzingatia Taratibu, Kanuni na Sheria kutoka Tshs. 3000/= iliyopo hadi Tshs. 1500/= upo katika mchakato huo wa uhuishaji wa Sheria ndogo, aidha katika makisio ya bajeti ya mwaka 2016/2017 kama tozo la kisheria kwa gunia la dagaa la Tshs. 3,000/= ipo katika utekelezaji wa bajeti.

9.3.6.1 Wajumbe waliupokea utekelezaji huo na kufunga hoja.

9.3.7 Kuhusu azimio Na. 7 la Muhtasari Na. HW/BRZ/2015-2016/06/7 Dondoo Na. 45.3.12.10 lilitekelezwa kwa Kaimu Afisa Rasilimali Watu (W), Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W) pamoja Mweka Hazina (W) kuwa katika kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kilimwagiza Mkurugenzi Mtendaji (W) kuwaagiza Mhandisi wa Ujenzi (W) na Mkadiriaji Majenzi (W) kufanya tathmini ya gharama zote katika ukamilishaji wa vyoo vya mnada wa Mwitende, mnada wa Namhula na mnada wa Buzimbwe na kuhakikisha fedha inatolewa ili kukamilisha ujenzi huo, hata hivyo tathmini ilifanyika na gharama za ukamilishaji ni Tshs. 6,250,000/=. Hatua za ukamilishaji wa vyoo vya mnada wa Mwitende, mnada wa Namhula na mnada wa Buzimbwe zinaendelea.

9.3.7.1 Aidha mchanganuo katika BOQ wa ukamilishaji wa vyoo hivyo uliwasilishwa kama ifuatavyo:-

- Mnada wa Mwitende – 3,000,000/=

- Mnada wa Namhula – 3,000,000/=

- Mnada wa Buzimbwe – 250,000/=

9.3.7.2 Wajumbe waliupokea utekelezaji huo japo hawakuridhishwa na matumizi ya fedha za awali kiasi cha Tshs 5,000,000/= zilizotolewa kujenga kila choo hii ni baada ya kubainika kuwa katika choo cha mnada wa Mwitende na Namhula katika mchanganuo uliowasilishwa wa ukamilishaji wa vyoo hivyo ni zaidi ya nusu ya fedha za awali.

9.3.7.7 Baada ya majadiliano ya muda mrefu wajumbe walitoa maazimio.

9.3.7.7.1 **AZIMIO.** Mkaguzi wa Ndani (W) afanye ukaguzi wa haraka wa fedha Tshs. 5,000,000/= zilizotolewa na Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa vyoo vya minada ya Mwitende, Namhula na Buzimbwe ikiwa kila choo kilitengewa kiasi hicho cha fedha. Aidha ukaguzi wa haraka ufanyike ili Mkurugenzi Mtendaji (W) aruhusu malipo ya Tsh. 3,250,000/= za ukamilishaji wa vyoo hivyo yafanyike ikiwa choo cha mnada wa Mwitende zitolewe Tsh. 1,500,000/=, mnada wa Namhula Tsh. 1,500,000/= na mnada wa Buzimbwe Tsh. 250,000/=.

9.3.7.7.2 **AZIMIO.** Mkurugenzi Mtendaji (W) amchukulie hatua za kinidhamu Mhandisi wa Ujenzi (W) kwa kushindwa kuandaa BOQ pamoja na kufanya makisio ya chini ya gharama za ujenzi Tsh. 5,000,000/= wa vyoo vya minada ya Buzimbwe, Mwitende na Namhula kwa kila choo na awawajibishe Watendaji wa Kata/Vijiji waliohusika kusimamia vyoo hivyo iwapo taarifa ya Mkaguzi wa Ndani (W) itathibitisha ubadhilifu wa fedha ulifanyika.

9.3.8 Kuhusu azimio Na. 8 la Muhtasari Na. HW/BRZ/2015-2016/06/7 Dondoo Na. 45.3.12.11 lilitokelezwa kwa Kaimu Afisa Rasilimali Watu (W) kuwa ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) ilimwandikia Mtendaji wa Kata ya Mugeta barua yenye Kumb. Na. HB/V:20/47/69 ya tarehe 06/09/2016 ya kumtaka kuhakikisha choo cha mnada wa Mugeta kinarejeshwa katika mamlaka ya Halmashauri na sasa choo hicho ni mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.

9.3.8.1 Wajumbe waliupokea utekelezaji huo na kufunga hoja hii ni baada ya Mhe. Diwani wa Kata ya Mugeta ambaye pia na Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Mugeta kuuhakikishia mkutano kuwa choo hicho tayari kinamilikiwa na Halmashauri, aidha alishauri kuwa ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) iwe inasoma mihtasari ya Vijiji inayoletwa Halmashauri.

9.3.9 Kuhusu azimio Na. 9 la Muhtasari Na. HW/BRZ/2015-2016/06/7 Dondoo Na. 45.3.13.5 lilitokelezwa kwa Mkurugenzi Mtendaji (W) kumwandikia barua Afisa Madini wa Kanda ya ziwa Victoria yenye Kumb. Na. HB/B:10/11/23 ya tarehe 01/11/2016 ya kumwomba kuhudhuria mkutano wa Baraza la Madiwani la tarehe 18/11/2016 ili kuja kutoa ufafanuzi kuhusu sekta ya Madini katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.

9.3.9.1 Kamishna wa Madini Kanda ya ziwa Victoria aliitikia agizo la Baraza la Madiwani kwa kuhudhuria mkutano huo ili kuweza kutoa ufafanuzi mbalimbali wa masuala ya sekta ya madini katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.

9.3.9.2 Wajumbe waliuliza maswali kwa Kamishna wa Madini Kanda ambapo walitaka yapate majibu ya kina.

9.3.9.3 Maswali yaliyoulizwa ni yafuatayo:-

- Katika Kata ya Nyamang'uta kuna Vijiji viwili vimebahatika kuwa na madini lakini kuna baadhi ya wawekezaji wamekuwa wakija na vibali wakidai kupewa vibali hivyo toka kwa Kamishna wa Madini Kanda, hata hivyo wawekezaji hao

wamekuwa wakienda moja kwa moja katika maeneo ya wananchi bila kufuata taratibu na kusababisha migogoro ya ardhi/mashamba (wananchi wa maeneo husika hawashirikishwi kuhusu ujio wa wawekezaji hao katika mashamba yao). Je kutokana na migogoro hiyo wananchi wa eneo husika, Kijiji husika na Halmashauri kwa ujumla vinanufaika vipi na uwepo wa wachimbaji hao?

- Ni vipi ofisi ya Kamishna wa Madini Kanda ya ziwa inatoa vibali vya uchimbaji wakati maeneo yenyewe haiyajui na kwa nini ofisi hizo hazimwelekezi (hapewi masharti) mwekezaji wa madini ya nini cha kufanya pale anapopewa kibali cha kuchimba madini maana wakifika eneo husika wanapoulizwa na viongozi wa eneo husika kinga yao huwa ni kuwa wamepata kibali toka kwa Kamishna wa Madini Kanda.

- Je Viongozi wa Vijiji wana uelewa na miongozo ya masuala ya uwekezaji wa madini?

- Je mtafiti wa madini anapewa miaka mingapi ya kufanya utafiti katika Halmashauri maana wamekuwa wakifanya shughuli za uchimbaji wa madini kama kawaida na wamekuwa wakichafua mazingira.

- Je ofisi ya Madini Kanda ya ziwa Victoria ipo tayari kuandamana na mteja wao (Mwekezaji wa Madini) pale wanapompata kibali cha kufanya utafiti au kuchimba madini katika Kijiji ili kuja kuwaeleza wananchi wa maeneo husika ili kuondoa tofauti na kero zinazojitokeza kati ya wawekezaji hao na wanakijiji.

- Je ni hatua gani zinazopaswa kuchukuliwa katika Halmashauri ambazo hazirejeshi 20% ya uchimbaji wa madini Vijijini?

- Je ni hatua gani zinachukuliwa na ofisi ya Madini Kanda ili kuhakikisha wananchi hawadhuriki na kemikali mbalimbali zitokanazo na shughuli mbalimbali za uchimbaji wa madini?

- Je ni lini Kamishna wa Madini Kanda ya ziwa Victoria atatembelea Kata za Butimba na Namhula ili kutatua changamoto za wachimbaji wa madini na wananchi zilizopo katika maeneo hayo?

9.3.9.4 Kamishna wa Madini Kanda ya ziwa Victoria alijibu maswali hayo kama ifuatavyo:-

9.3.9.4.1 Kwa mujibu wa Sheria Na. 14 ya mwaka 2010 imeeleza kuwa Mtanzania yeyote mwenye akili timamu aliyefikisha umri wa miaka 18 anapokuja kuomba kibali cha kuwekeza katika sekta ya madini anaruhusiwa kupewa kibali hicho, anapaswa kuripoti katika uongozi wa Kijiji anapoenda kuwekeza na haruhusiwi kuchimba hadi hapo atakapokuwa amefanya makubaliano na mwenye shamba/ardhi. Aidha alieleza kuwa wapo baadhi ya wananchi wanaopenda kufanya nao kazi na wengine wanapenda kupewa fidia ya ardhi kama ilivyoelekeza katika kifungu Na. 5 cha Sheria ya Ardhi.

9.3.9.4.2 Halmashauri mara nyingi hunufaika na uwepo wa wawekezaji wenyewe lakini pia inanufaika na kupata ushuru wa huduma ambapo ni wajibu wa Halmashauri kurejeshi 20% ya mapato yatokanayo na wachimbaji hao ya

- ushuru wa huduma katika Kijiji husika.
- 9.3.9.4.3 Ofisi ya Madini Kanda huwa inawafahamisha wawekezaji wa madini wote wanaokuja kuchukua leseni ya uwekezaji katika sekta ya madini kuyasoma na kuyaelewa masharti ya uwekezaji na inawasainisha fomu zenye masharti hayo ambazo zinapatikana katika ofisi za Madini Kanda, ofisi itajitahidi kuziwasilisha fomu hizo katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) kwa ajili ya utekelezaji zaidi. Ni jukumu la Halmashauri kuwaeleza Watendaji wake wa Kata na Vijiji juu ya kufuatilia fedha za ushuru wa huduma zitokanazo na wachimbaji hao.
- 9.3.9.3.4 Kuhusu suala la uchafuzi wa mazingira linalosababishwa na wachimbaji na watafiti wa madini katika Vijiji, Kamati za Usafi za Kata/Vijiji zinapaswa kuchukua hatua kwa kuwaeleza wachimbaji hao athari wanazozisababisha kwa wananchi lakini pia kuwasiliana na ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) na ikiwezekana kuifahamisha ofisi ya Madini Kanda ili kuchukua hatua zaidi dhidi ya wachimbaji hao.
- 9.3.9.3.5 Kuhusu suala la ofisi ya Madini Kanda ya ziwa Victoria kuandamana na mteja wao (Mwekezaji wa Madini) pale wanapompata kibali cha kufanya utafiti au kuchimba madini katika Kijiji, ofisi iko tayari lakini ifahamike kuwa ni gharama kubwa zinazohitajika na zinahitaji bajeti.
- 9.3.9.3.6 Alitoa ufafanuzi juu ya Halmashauri kutorejeshwa 20% ya mapato yatokanayo na uchimbaji wa madini (fedha za ushuru wa huduma) kurudi katika Kijiji husika Sheria iko kimya na haijazungumzia chochote juu ya kuibana Halmashauri kuhakikisha inarudisha asilimia hizo zitokanazo na ushuru wa huduma. Alisema kuwa ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) inaweza kuwaandikia barua ya kuomba kuwapatia takwimu za bei za mauzo (turnover) za wachimbaji wa madini walioko Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.
- 9.3.9.3.7 Taratibu za kupata leseni kwa wachimbaji wa madini zinafuatwa kwa kuzingatia Sheria ya madini Na. 19 ya mwaka 1979 na zinaelekeza kuwa mchimbaji wa madini anapopata kibali cha uchimbaji anapaswa kupita kwa Mkuu wa Wilaya ili kupata maelekezo pia anaenda kwa viongozi wa Vijiji kwa ajili ya utambulisho. Aidha, mfumo wa kuomba kibali cha kuwekeza katika sekta ya madini umekuwa wazi ambapo wawekezaji wamepata fursa ya kuomba vibali kupitia mtandaoni (online system).
- 9.3.9.3.8 Sheria ya madini Na. 17 ya mwaka 1979 imefafanua kuwa mwekezaji anayefanya utafiti, atafanya utafiti kwa muda wa miaka 7 tu na hapo hatoruhusiwa kufanya utafiti katika maeneo hayo ila kwa sasa Sheria hiyo imebadilishwa kwa kuwaongezea watafiti wa madini hadi kwa muda wa miaka 9 kufanya utafiti huo. Kazi kubwa ya watafiti wa madini huwa ni kubaini aina ya madini yapatikanayo katika eneo husika kwa kuchukua sampuli ya madini hayo katika maabara ambapo ndipo itathibitika kuwa katika eneo hilo kuna madini ya aina fulani.
- 9.3.9.3.9 Siku uongozi wa Kata ya Butimba pamoja na Namhula ukiwa tayari utaijulisha ofisi ya Madini Kanda ili ije katika Kata hizo kutatua changamoto zilizopo kati wawekezaji na wananchi.

- 9.3.9.3.11 Ofisi za Kata na Vijiji zinao wajibu wa kukusanya takwimu za uzalishaji wa madini katika maeneo ya wachimbaji walioko katika maeneo yao. Aidha alieleza kuwa watafiti wa madini ni wadanganyifu sana kueleza kile wanachokizalisha na alishauri kuwa Watendaji wa Kata na Vijiji kufanya ukaguzi wa nini kinafanyika na kuchukua takwimu za uzalishaji unaoendelea katika maeneo hayo.
- 9.3.9.3.12 Aliwaomba Wahe. Madiwani kutoa ushirikiano wa kina ili kusaidia zoezi linaloendelea kwa sasa la ukusanyaji wa ushuru wa madini ya ujenzi ambapo kwa kila roli ni Tshs. 3,000/= na madini ya kokoto kwa roli ni Tshs. 6,000/= na Halmashauri inaweza kumteua mtumishi wa kuweza kusimamia zoezi hilo ambapo itafaidika na ushuru wa huduma pamoja na mrabaha wa madini ya ujenzi.
- 9.3.9.3.13 Mhe. Kangi Lugora Mbunge wa Jimbo la Mwibara alitoa uzoefu katika sekta ya madini, akieleza kuwa katika sekta zinazosababisha migogoro mingi hapa nchini ni pamoja na sekta ya madini ambapo wawekezaji wengi huwa na lugha ya utafiti wakati nia yao ni kufanya uchimbaji wa madini. Hii huleta migogoro kwa kuwa eneo moja hufanyiwa utafiti na mwekezaji mmoja kwa kutumia majina tofauti na kwa vipindi tofauti hivyo kukuta eneo hilo linafanyiwa utafiti zaidi ya miaka 20 jambo ambalo huleta kero kubwa kwa wananchi. Hata hivyo kinachowaumiza zaidi wananchi ni kitendo cha watafiti hao kuchimba madini kawaida kama wachimbaji wenye vibali vya kuchimba madini na Halmashauri hushindwa kuwadai ushuru wa huduma.
- 9.3.9.3.14 Baada ya maelezo mazuri ya Kamishna wa Madini Kanda wajumbe walitoa ushauri mbalimbali kama ifuatavyo:-
- 9.3.3.14.1 **USHAURI.** Ofisi ya Madini Kanda iwe inaziwasilisha kwa Mkurugenzi Mtendaji (W) mapema nakala za fomu za masharti kwa mwekezaji wa madini aliyepata kibali cha kuwekeza katika Halmashauri ili kuweza kuyapitia masharti hayo kinagaubaga kabla ya mwekezaji huyo kuja katika Halmashauri.
- 9.3.3.14.2 **USHAURI.** Ofisi ya Madini Kanda ione umuhimu wa kuwaandikia barua wawekezaji na watafiti wote wa madini wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda kuwakumbusha kufuata Taratibu, Kanuni na Sheria za uchimbaji wa madini hii ni pamoja na kuwataka kulipia ushuru wa huduma katika Halmashauri.
- 9.3.3.14.3 **USHAURI.** Afisa Madini Kanda awasilishe Halmashauri takwimu sahihi za mauzo ya wachimbaji wa madini ya Halmashauri ili kuweza kudai ushuru wa huduma kwa wachimbaji wa madini.
- 9.3.10 Kuhusu azimio Na. 10 la Muhtasari Na. HW/BRZ/2015-2016/06/8 Dondoo Na. 46.1.2.2.1 lilitekelezwa kwa Mhe. Jogoro A. Biswalo Mwenyekiti wa Kamati ndogo kuwasilisha taarifa ya ziara ya Kamati ndogo ya kutembelea na kukagua mradi wa maji wa Mugeta/Nyang'aranga kwa upande wa Kijiji cha Mugeta kama unatoa maji kuwa Kamati ndogo iliteuliwa na Baraza la Wahe. Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda tarehe 19/08/2016 ilifanya

ziara ya kutembelea na kukagua mradi wa maji Mugeta/Nyang'aranga kwa upande wa Kijiji cha Mugeta ulioko Kata ya Mugeta Halmashauri ya Wilaya ya Bunda tarehe 24/10/2016. Katika ziara hiyo Kamati ndogo ilitembelea pia DP mbili (02) zilizopo sehemu ya Kijiji cha Nyang'aranga ambazo zinapata maji kutoka chanzo cha maji kilichopo Kijiji cha Mugeta.

9.3.10.1 Mradi wa maji wa Vijiji vya Mugeta na Nyang'aranga ulibuniwa kwa ushirikiano kati ya wananchi na Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ili kujibu kero ya muda mrefu ya maji kwa ajili ya binadamu na mifugo kwa kuwa Vijiji hivyo havina mto na ziwa Victoria lipo umbali wa 80km.

9.3.10.2 Vijiji vya Mugeta na Nyang'aranga ni Vijiji vya wakulima na wafugaji. Vijiji hivyo vina jumla ya wakazi 6,624 (Mugeta 2,336 na Nyang'aranga 4,288) na Ng'ombe wapatao 3,600.

9.3.10.2 Utekelezaji wa mradi wa maji wa Mugeta/Nyang'aranga.

9.3.10.2.1 Mradi huo ulianza mwaka 2009 kwa kuja wataalam washauri kwa ajili ya kutambulisha mradi katika Vijiji vya Mugeta/Nyang'aranga.

Mradi huu ulitakiwa utekelezwe kwa gharama ya Tshs. 495,145,715.14 kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kwa mkataba LGA/065/2011-2012/W/WSDP/1-3, Lot Na. BD-C9 uliosainiwa tarehe 30/05/2012 fedha za Benki ya Dunia.

NB: Lakini kutokana na mchakato wa ufadhiri wa Benki ya Dunia kwa miradi ya maji kuchukua muda mrefu, katika kuleta fedha/kufadhiri miradi hiyo aliyekuwa Mhe. Mbunge wa Jimbo la Bunda Ndg. Stephen Masatu Wasira aliwasilisha andiko la mradi kwenye Ubalizi wa Japan la kuomba fedha za ujenzi wa mradi Kijiji cha Mugeta peke yake kutokana na kilio kikubwa cha wananchi wa Kijiji cha Mugeta kuhusu uhaba zaidi wa maji kwa kipindi hicho.

Andiko hilo la mradi liliomba Tshs. 270,000,000/= lenye mchanganuo ufuatao:-

NA.	CHANZO CHA FEDHA	KIASI
1.	Japan	240,000,000/=
2.	Halmashauri	23,000,000/=
3.	Wananchi	7,000,000/=
	JUMLA KUU	270,000,000/=

9.3.10.2.2 Mpaka tarehe ya utekelezaji wa mradi huu ni kiasi cha fedha Tshs. 210,000,000/= ndizo zilipokelewa toka Serikali ya Japan.

9.3.10.2.2 Halmashauri ilitoa kiasi cha fedha Tshs. 3,015,000/= kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa maji chini ya ardhi. Wananchi wa Kijiji cha Mugeta hawakutoa chochote kama mchango wao.

9.3.10.3 Hali halisi ya maji ya Mugeta/Nyang'aranga

9.3.10.3.1 Hali halisi ya mradi wa maji Mugeta/Nyang'aranga kwa upande wa Kijiji cha Mugeta ni nzuri kwani DP 07 zinatoa maji na DP 02 kwa upande wa Kijiji cha Nyang'aranga zinatoa maji, isipokuwa DP 01 iliyopo eneo la Manyangare, DP hiyo kwa mujibu wa maelezo ya Mhandisi wa Maji na udhibiti wa Maji Taka

(W) ilijengwa kimakosa na Mkandarasi wala haimo katika BOQ na haikulipwa, aidha maelezo hayo yalithibitishwa na Mkandarasi wa mradi wa maji Mugeta/Nyang'aranga aliyefanya kazi hiyo.

9.3.10.4 **Changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi.**

9.3.10.4.1 **Kuchelewa kupokelewa kwa fedha za umeme.**

9.2.10.4.1.1 Tatizo kubwa lililojitokeza katika mradi huu ilikuwa ni ukosefu wa fedha na kuchelewa kwa kupokelewa kwa fedha kwa ajili ya kusambaza umeme. Kwa sababu hiyo mkandarasi alilazimika kukabidhi mradi huo Halmashauri kabla ya kukamilika hii ikiwa ni pamoja na kufanya majaribio ya miundombinu ya maji na kuweka dawa katika mifumo ya maji.

Mkandarasi huyo aliamua kukabidhi mradi huo kwa Halmashauri ili kuepuka gharama ambazo angekutana nazo bila kujua ni lini fedha za umeme zingepatikana.

NB: Miundombinu ya maji ilikamilika tarehe 02/02/2013 na kukabidhiwa kwa Halmashauri tarehe 30/05/2013 baada ya kusubiri fedha ya umeme kwa miezi mitatu bila mafanikio.

9.2.10.5 **Mapendekezo ya Kamati.**

- (i) Huduma ya maji inayopatikana katika Vijiji vya Mugeta na Nyang'aranga ilipiwe ili kukidhi gharama za uendeshaji wa mradi. Aidha ziwepo Kamati ndogo za maji kwa ajili ya usimamizi wa mradi.
- (ii) Pamoja na kwamba DP iliyojengwa kimakosa eneo la Manyangare haikuwemo katika BOQ Kamati inapendekeza Serikali ijitahidi kupeleka maji kwani kuna uhitaji mkubwa wa huduma hiyo.
- (iii) Kwa wale wananchi waliojenga na kulima katika maeneo ya miundombinu ya maji Kamati inapendekeza Serikali za vijiji husika ichukue hatua za maksudi za kuwaondoa wananchi wote waliovamia miundombinu ya maji.
- (iv) Mkandarasi asawazishe matuta kwenye maeneo aliyochimba mitaro ya mabomba kwa trench digger.
- (v) Serikali itafute fedha kwa ajili ya kukarabati miundombinu iliyoharibika kipindi cha 2013-2016 kwa ajili ya kijiji cha Nyang'aranga ili wananchi wa eneo hilo wapate huduma ya maji.
- (vi) Mtaalam mshauri na mkandarasi mjenzi Audacia Investment Ltd waeleze sababu za kujenga DP 20 badala ya DP 25 kwa mujibu wa mkataba.
- (vii) Kamati inapendekeza ukaguzi wa mradi wa maji Mugeta/Nyang'aranga ufanyike kwani fedha zilizotumika ni nyingi ukilinganisha na hali halisi ya utekelezaji wa mradi.

9.2.10.6 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, walijadili kwa kina huku wakijadili zaidi mapokezi ya fedha katika awamu ya III ya fedha toka Ubalazi wa Japan Tshs. 210,000,000/= zilizofunguliwa akaunti namba 3011200116 katika ngazi ya Halmashauri na zilitumika kufanya kazi kwa kutumia wakandarasi watatu (3) ambapo mkandarasi wa pili Contrive Engineering mkataba wake ulikuwa ni wa kiasi cha Tshs. 81,407,500/= mkataba Na. LGA: 065/2009-2010/W/JICA/08 na alipewa tenda ya kujenga tenki la maji lenye ujazo wa lita laki moja na hamsini elfu (150,000) ila kutokana na hali ya udongo kutoweza kuhimili

kubeba tanki la lita 150,000 ililazimika kukubalika kujenga tanki lenye ujazo wa lita 100,000 za maji lenye thamani ya kiasi cha fedha Tshs. 71,258,809/= ambapo wajumbe walitaka kupata namba ya mkataba huo (namba ya mkataba haikuonekana/haikuwasilishwa).

9.2.10.7 Walimjadili pia mkandarasi wa tatu Audacia Investment L.t.d aliyepewa tenda ya kuchimba mtaro wa bomba, kujenga DP na kununua mabomba ya kazi hiyo kwa gharama ya Tshs. 119,211,191/= ambapo pia namba ya mkataba haikuoneshwa (namba ya mkataba haikuonekana/haikuwasilishwa).

9.2.10.8 Aidha wajumbe walijadili pia mapokezi ya fedha katika awamu ya tano ya mradi ambapo mradi uliitaji umeme kwa ajili ya kusukuma maji katika maeneo yote ya mradi wa maji, baada ya Wizara ya Maji kupitia Benki ya Dunia WSDP kuchelewa kuleta fedha kiasi cha Tshs. 119,275,844/= zilizokuwa katika mkataba, aliyekuwa Mhe. Mbunge wa Jimbo la Bunda Ndg. Stephen Masatu Wasira alijitahidi kutafuta fedha kwa ajili ya kusambaza umeme.

9.2.10.8.1 Katika jitihada zake alifanikiwa kupata kiasi cha fedha Tshs. 125,000,000/= kutoka Wizara ya Nishati na Madini kupitia mradi wa umeme vijijini (REA).

9.2.10.8.2 Fedha hizo zilipokelewa na kuingia kwenye akaunti ya maendeleo ya Halmashauri (Development Cash Account), wajumbe pia walitaka kupata akaunti namba ambayo fedha hizo ziliingizwa (akaunti Na. haikuwasilishwa).

9.2.10.9 Baada ya majadiliano ya kina wajumbe walitoa azimio.

9.2.10.9.1 **AZIMIO.** Mkaguzi wa Ndani (W) afanye ukaguzi wa matumizi ya fedha zote zilipokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji wa Mugeta/Nyang'aranga katika awamu mbalimbali.

9.2.11 Kuhusu azimio Na. 11 la Muhtasari Na. HW/BRZ/2015-2016/06/8 Dondoo Na. 46.1.4.8.1 lilitekelezwa kwa Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W) kueleza kuwa ofisi ya Mifugo na Uvuvi iliandaa utaratibu na iliutangaza mnada wa Hunyari ambapo tayari ulishaanzishwa toka mwezi wa 9/2016 na unafanyika kila tarehe 9 ya kila mwezi.

9.2.11.1 Wajumbe waliupokea utekelezaji huo na kufunga hoja.

MUHTASARI NA. HW/BRZ/2016-2017/01/7 TAARIFA ZA KAMATI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI.

10.1 Taarifa za Kamati za Kudumu za Halmashauri ziliwasilishwa kwenye mkutano huo kama ifuatavyo:-

10.1.1 (i) Taarifa ya Kamati ya Kudhibiti UKIMWI robo ya I mwaka 2016/2017.

10.1.1.1 Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye mkutano na Mhe. Godliver Masamaki kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri.

10.1.1.2 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, walijadili na kuipitisha baada ya kutoa ushauri kuwa Mwenyekiti wa Halmashauri na Katibu wa Vikao vya Halmashauri (Mkurugenzi Mtendaji Wilaya) waone umuhimu wa kuwaongeza

wajumbe wa Kamati ya Kudhibiti UKIMWI kwenye Kamati za kudumu za Halmashauri hii ni pamoja na kuongeza wajumbe wengine wawili (02) kwenye Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kama ilivyotafsiliwa kwenye mwongozo wa Uundaji wa Kamati za Halmashauri wa tarehe 10/11/2016 uliotolewa na Katibu Mkuu.

10.1.2 (ii) Taarifa ya Kamati ya Elimu, Afya na Maji robo ya I mwaka 2016/2017.

10.1.2.1 Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye mkutano na Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Misana S. Jigwila.

10.1.2.2 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, waliijadili na waliipitisha baada ya kutoa ushauri na maazimio mbalimbali kama ifuatavyo:-

10.1.2.2.1 **USHAURI.** Halmashauri ione umuhimu wa kupeleka watumishi wa Afya katika zahanati za Igundu na Iramba ikiwa baadhi ya watumishi katika zahanati hizo walitoroka kutokana na zoezi linaloendelea la kuhakiki watumishi hewa.

10.1.2.2.2 **USHAURI.** Halmashauri itenge fedha za kuimarisha vituo vya Afya vya Kasahunga na Ikizu.

10.1.2.2.3 **AZIMIO.** Mhandisi wa Ujenzi (W) afanye tathmini (makisio) ya ujenzi wa choo katika Kituo cha Afya Ikizu ikiwa wananchi wa Kata ya Nyamuswa walishajitolea kuchimba mashimo na kujenga boma katika choo hicho.

10.1.2.2.4 **USHAURI.** Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) ione umuhimu wa kutenga fedha za ukarabati wa ofisi ya Maendeleo ya Jamii.

10.1.2.2.5 **AZIMIO.** Mkurugenzi Mtendaji (W) amwajibishe mfadhili tapeli aliyejifanya kutokea Kampuni ya Vodacom Foundation na kusababisha maafa makubwa katika Kata za Butimba, Kasuguti na Nyamihyolo kwa kubomoa vyumba vya madarasa kumtaka kujenga vyumba hivyo haraka iwezekanavyo kwa gharama zake mwenyewe.

10.1.3 (iii) Taarifa ya Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira robo ya I mwaka 2016/2017.

10.1.3.1 Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye mkutano na Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Keremba J. Irobi.

10.1.3.2 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, waliijadili na waliipitisha baada ya kutoa ushauri mbalimbali kama ifuatavyo:-

10.1.3.2.1 **USHAURI.** Halmashauri itafute namna ya kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya Nyamuswa maana tumekuwa tukikosa mapato mengi katika stendi hiyo.

10.1.3.2.2 **USHAURI.** Halmashauri ione umuhimu wa kujenga vizimba vya kukusanyia taka katika Kata ya Nyamuswa maana viko katika bajeti tunayoendelea nayo ya mwaka 2016/2017.

10.1.3.2.3 **USHAURI.** Kuhusu suala la kurejesha 20% vijijini ya ukusanyaji wa mapato ilijadiliwa na kushauriwa kurejeshwa kwenye Kikao cha Fedha,

Uongozi na Mipango ili lijadiliwe zaidi.

10.1.4 (iv) Taarifa ya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango robo ya I mwaka 2016/2017.

10.1.4.1 Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye mkutano na Mhe. Kerembe J. Irobi kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri.

10.1.4.2 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, waliijadili na waliipitisha baada ya kutoa ushauri mbalimbali kama ifuatavyo:-

10.1.4.2.1 **USHAURI.** Mkurugenzi Mtendaji (W) aitische mkutano maalum wa Baraza la Madiwani la kujadili hoja za Mkaguzi na Mdhambi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuwa mkutano huo upo kwa mujibu wa Sheria.

10.1.4.2.2 **USHAURI.** Menejimenti ihakikishe kuwa fedha za makusanyo 60% zinaelekezwa katika miradi ya maendeleo na 40% zitumike katika uendeshaji wa Halmashauri.

10.1.4.2.3 **USHAURI.** Menejimenti ihakikishe inaweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha inaziba mianya ya upotevu wa mapato ya Halmashauri.

10.1.4.2.4 **USHAURI.** Menejimenti itenge fedha kwa ajili ya ujenzi wa choo kingine katika mnada wa Mugeta.

10.1.4.2.5 **USHAURI.** Menejimenti ihakikishe inaharakisha mchakato wa ukarabati wa lambo la Kisangwa.

10.1.5 Wajumbe walijadili zaidi juu ya dondoo Na. 109.4.3 hadi 104.4.3.3.1 iliyowasilishwa na wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ya kuomba idhini ya kubinafsisha baadhi ya vyanzo vya mapato ya Halmashauri katika upande wa minada. Taarifa iliyowasilishwa kwenye mkutano ikiomba idhini ya kubinafsisha chanzo hicho cha mapato ya minada ni kama ifuatavyo:-

- Mnada wa Mwitende mzabuni awe analeta Tshs. 400,000/= kwa mwezi
- Mnada wa Namhula mzabuni awe analeta Tshs. 1,000,000/= kwa mwezi.
- Mnada wa Mihingo mzabuni awe analeta Tshs. 200,000/= kwa mwezi.
- Mnada wa Bulamba mzabuni awe analeta Tshs. 1,000,000/= kwa mwezi.
- Mnada wa Mugeta mzabuni awe analeta Tshs. 10,000,000/= kwa mwezi.

10.1.5.1 Baada ya wajumbe kufanya ulinganifu yakinifu na kujiridhisha juu ya ukusanyaji wa mapato katika minada kati ya wazabuni na Halmashauri kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai hadi Septemba, 2016 hawakuridhia kubinafsisha chanzo hicho, wakieleza kuwa Halmashauri bado inafanya vizuri katika ukusanyaji ukilinganisha na wazabuni hivyo hakuna sababu yoyote ya kubinafsisha chanzo hicho. Ilisisitiza kuwa Halmashauri iweke mpango mkakati madhubuti wa ukusanyaji wa mapato.

MUHTASARI NA. HW/BRZ/2016-2017/01/8 TAARIFA MBALIMBALI.

11.1 (i) Matumizi ya magari ya Halmashauri.

11.1.1 Taarifa hiyo iliwasilishwa na kusomwa kwenye mkutano na Kaimu Afisa Rasilimali Watu (W) kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W) kuwa Mhandisi

Mussa I. Iyombe Katibu Mkuu aliwaandikia barua Wakurugenzi wote nchini wa Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Halmashauri za Wilaya yenye Kumb. Na. CB.215/402/01/186 ya tarehe 12/10/2016 kuhusu matumizi ya Magari ya Halmashauri.

- 11.1.2 Katika siku za hivi karibuni, ofisi ya Rais – TAMISEMI imekuwa ikipokea maombi mbalimbali ya magari kutoka kwa Wakurugenzi wa Halmashauri. Pamoja na sababu nyinginezo, uchakavu wa magari umetajwa kuwa ni mojawapo ya visababishi vya upungufu wa magari katika Halmashauri.
- 11.1.3 Uchunguzi uliofanywa na ofisi ya Rais – TAMISEMI umebaini kuwa uchakavu wa magari ya Halmashauri unatokana na matumizi mabaya ya magari kwa Maafisa walipewa dhamana ya kuyatumia magari hayo. Ipo tabia ya Viongozi wa Kisiasa na watumishi wa Halmashauri kwa shughuli zao binafsi. Hali hii inasababisha viongozi hao kuchagua ama kupendekeza kuendesha na baadhi ya madereva ambao wanawza kutekeleza matakwa yao na kuwataka madereva ambao wanasimamia na kutekeleza maadili ya taaluma zao na Utumishi wa Umma.
- 11.1.4 Katibu Mkuu aliwaagiza Wakurugenzi wa Halmashauri wote kusimamia ipasavyo matumizi ya magari pamoja na mali nyingine za Halmashauri na kuhakikisha kuwa zinatumiwa kwa maslahi ya Umma. Safari zote za kikazi za viongozi wa Kisiasa na Watendaji Wakuu na watumishi ziratibiwe kwa Mujibu wa Kanuni na miongozo iliyopo kuhusu uendeshaji wa shughuli za Halmashauri na kumbukumbu za safari zote za kikazi ziwekwe kwenye kitabu cha safari (log book). Kanuni za Halmashauri zisomwe, zitafsiriwe na zieleweke kwa viongozi wa Kisiasa na watumishi wote wa Halmashauri ili zitekelezwe kikamilifu.
- 11.1.5 Aidha, upangaji wa magari kwa madereva uzingatie weledi wa taaluma ya mtumishi na siyo kwa upendeleo au kwa maslahi binafsi ya Kiongozi husika. Ofisi ya Rais – TAMISEMI haitasita kumchukulia hatua za kinidhamu na za kisheria Kiongozi au mtumishi yeyote atakayebainika kukiuka Kanuni za Halmashauri, Taratibu na Maadili ya Utumishi wa Umma kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya mwaka 1995 na Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002.
- 11.1.6 Aliwataka, barua hii isomwe kwenye Mabaraza ya Madiwani kwa kuwa Waheshimiwa Madiwani ndiyo wasimamizi wakuu wa mali za Halmashauri ili wao wenyewe waongoze katika utunzaji wa mali za Halmashauri na waweze kusimamia ipasavyo utekelezaji wa maelekezo hayo.
- 11.1.7 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuipitisha kwa utekelezaji.

MUHTASARI NA. HW/BRZ/2015-2016/01/09 KUFUNGA MKUTANO.

- 12.1 Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afunge mkutano.
- 12.2 Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe wote kwa michango yao ya mawazo na kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa manufaa ya Halmashauri.

12.2.1 Aliwaomba wajumbe kuwa na mawazo ya pamoja wakati wa kufanya maamuzi mbalimbali watakapojigeuza Kamati kujadili masuala ya watumishi kwa mujibu wa kifungu na 34 na 35 cha Kanuni za kudumu za mikutano ya shughuli za Halmashauri zilizotungwa chini ya Kifungu cha 70 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Na. 7 ya mwaka 1982 vimeipa mamlaka Baraza la Madiwani kujigeuza kama Kamati endapo litajitokeza jambo lolote katika kikao cha Halmashauri linalohusu uteuzi, kupandishwa cheo, kufukuzwa kazi, mishahara au mazingira ya kazi au utendaji kazi kwa jumla wa mtumishi yeyote wa Halmashauri, jambo hilo litajadiliwa katika Kamati ya Halmashauri nzima, isipokuwa kama Halmashauri itaamua vinginevyo.

12.2.3 Alifunga mkutano saa 11:13 jioni.

UMETHIBITISHWA.

SAINI YA MWENYEKITI.....SAINI YA KATIBU.....

JINA LA MWENYEKITI.....JINA LA KATIBU.....

TAREHE.....